



**Tangazo kwa Vyombo vyahabari**  
**Kusitisha Majukumu ya Ndugu Alaa Abu Saleh katika Afisi ya Habari**  
**(Imetafsiriwa)**

Bismillahi Ar-Rahman Ar-Rahim

Alhamdulilah, rehma na amani zimshukie Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw),

Kwanza, napenda kutoa shukrani zangu kwa Amiri wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni mkubwa, Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah, Mwenyezi Mungu amhifadhi, kwa amana na fursa aliyonipa kufanya kazi ndani ya Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Ardhi Iliyobarikiwa - Palestina katika kipindi cha miaka iliyopita. Nimemuomba Mwenyezi Mungu (swt) aifanye juhud yangu ya unyenyekevu kuwa mchango katika mradi wa mwamko wa Ummah na kuifanya kuwa ya iklasi kwa ajili ya kazi Yake tukufu. Namuomba (swt) awape Waislamu ushindi na tamkini kwa kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume. Khilafah ambayo itaikomboa Masra, wafungwa wa kivita na kuwaletea ushindi watu wa Gaza na Palestina, na kulipiza kisasi kwa wakoloni wote waliosubutu kuwashambulia Waislamu, kuikalia kwa mabavu ardhi yao, na kuinajisi Masra ya Mtume wao (saw).

Zaidi ya hayo, natangaza kusitisha kazi yangu katika Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Ardhi Iliyobarikiwa - Palestina, ili kutoa nafasi kwa nguvu changa zinazoingiza uchangamfu na mng'aro, na kuiingiza kazi hii damu mpya na mbinu mbalimbali. Namuomba Mwenyezi Mungu (swt) kwa ajili ya ndugu zangu katika Afisi ya Habari mafanikio na ustawi, na kwamba daima wawe ni sauti kubwa ya kutangaza haki, na kwamba kheri itiririke mikononi mwao. Kutowana na haya, hii ni taarifa kwa vyombo vyahabari inayosema kwamba sina tena uwezo rasmi wa kuzungumza na vyombo vyahabari.

Salamu za dhati,

**Alaa Abu Saleh**

Kwa upande wetu sisi katika Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Ardhi Iliyobarikiwa – Palestina, tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) azikubali juhud za Ustadh Alaa Abu Saleh na amlipe malipo tele kwa kazi zote alizozifanya katika miaka aliyohudumu katika Afisi hii ya Habari.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**  
**katika Ardhi Iliyobarikiwa – Palestina**